

TANZANIA / JUDGMENT

MGAMBWA SADALA MCHIWA

COURT
TANZLII

DECIDED
1 January 2024

Source: media.tanzlii.org · Research copy typeset by Esheria. Not court-issued or certified.

KATIKA MAHAKAMA KUU YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA (MASIJALA NDOGO YA DODOMA) ILIYOPO DODOMA MAOMBI MADOGO YA JINAI Na. 23808 YA 2024 (AsiHa shauri la Uhujumu Uchumi Namba 12 la 2023, Mahakama ya WHaya ya Manyoni) MGAMBWA SADALA MCHIWA @ MUSSA SADALA MCHIWA..... MLETA MAOMBI DHIDI YA JAMHURI..... MJIBU MAOMBI UAMUZI Tarehe ya amri ya mwisho: 26/9/2024 Tarehe ya uamuzi: 30/9/2024 KHALFAN, J. Mgambwa Sadala Mchiwa, mleta maombi katika shauri hili, ameleta maombi haya chini ya kifungu cha 361(2) cha sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai [Sura ya 20 marejeo ya mwaka 2022]. Mleta maombi anaomba mahakama hii imuongezee muda zaidi ili aweze kuleta taarifa ya nia ya kuleta rufaa na rufaa nje ya muda dhidi ya hukumu ya mahakama ya wilaya ya Manyoni katika shauri la Uhujumu Uchumi namba 12 la mwaka

2023. Maombi haya yameambatishwa na kiapo cha mleta maombi. i Maombi haya yalipoitishwa kwa ajili ya kusikilizwa, mleta maombi alifika na hakuwa na uwakilishi wowote. Upande wa mjibu maombi uliwakilishwa na Bi. Zubeda Lyaumi na Bi. Linda Mmbaga, mawakili wasomi wa serikali. Alipopewa nafasi ya kufanya mawasilisho yake, mleta maombi aliomba mahakama izingatie kiapo chake kama sehemu ya mawasilisho yake. Hakuwa na jambo la ziada la kuieleza mahakama. Kwa upande wake, Bi. Lyaumi, wakili msomi wa serikali, aliunga mkono maombi haya. Aliieleza mahakama kwamba mleta maombi ana sababu ya msingi ambayo imeainishwa katika aya ya nne (4) ya kiapo chake. Alieleza kwamba, baada ya kutiwa hatiani na kupewa adhabu ya kifungo, mleta maombi alikata rufaa katika mahakama hii. Alieleza zaidi kwamba, rufaa hiyo ilipoitishwa kwa ajili ya kusikilizwa mleta maombi aliomba kuondoa rufaa yake kwa kuwa ilikuwa na mapungufu kadhaa. Alieleza kwamba, rufaa ya mleta maombi iliondolewa tarehe 22/4/2024. Alieleza kwamba kwa kuwa mleta maombi yupo gerezani ambapo hutegemea zaidi maafisa wa magereza katika kuandaa nyaraka kumepelekea mleta maombi kushindwa kuleta rufaa yake kwa wakati. Wakili 2 msomi wa serikali alieleza kwamba, rufaa ni haki ya kila mmoja ambaye hajaridhika na maamuzi ya mahakama. Hivyo, ili haki iweze kutendeka, mleta maombi aruhusiwe kuleta rufaa yake. Baada ya kupitia majumuisho ya pande zote mbili katika maombi haya, jambo la msingi ni endapo mleta maombi ametoa sababu za msingi katika maombi haya. Ingawa maombi haya hayakupingwa na mjibu maombi, mahakama bado ina jukumu la kupima endapo mleta maombi ana sababu za msingi. Msimamo huu

ulielezwa katika shauri la Karibu Textile Mills Limited dhidi ya Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania maombi madogo ya Madai Na. 192/20 ya 2016 Mahakama ya Rufaa ya Tanzania iliyoketi Dar es Salaam (haijaripotiwa). Kama ilivyoelezwa hapo awali, maombi haya yameletwa chini ya kifungu cha 361(2) cha sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai. Kifungu hicho kinaipa mahakama hii mamlaka ya kuongeza muda wa kukata rufaa pale ambapo sababu za msingi zinakuwa zimetolewa. Katika maombi haya ambapo kimsingi yaliungwa mkono na wakili msomi wa serikali, ni kwamba mara baada ya uamuzi wa mahakama ya Wilaya kutolewa, mleta maombi alifungua rufaa katika mahakama hii, lakini rufaa hiyo iliondolewa na mleta maombi baada ya kuwa na dosari kadhaa. Alieleza kwamba mleta maombi yupo gerezani ambapo anategemea mamlaka ya gereza imsaidie kuandaa nyaraka zake kwa ajili ya rufaa jambo lililopelekea kuchelewa kufungua rufaa yake. Baada ya kupitia hoja za pande zote mbili pamoja na kiapo cha mleta maombi, ni wazi kwamba mleta maombi ameweza kuainisha sababu za msingi za kuchelewa kwake kufungua rufaa kwa wakati. Katika shauri hili, imeelezwa wazi kwamba mleta maombi alifungua rufaa yake katika mahakama hii lakini ilionekana kuwa na dosari na hivyo kuondolewa tarehe 22/4/2024. Hata hivyo, nimezingatia kwamba mleta maombi yupo gerezani kunakomfanya awe tegemezi kwa maafisa wa magereza kuandaa nyaraka zake za rufaa. Kwa sababu hiyo, mahakama inaona maombi haya yana mashiko hivyo inayakubali. Mleta maombi alete taarifa ya nia ya kukata rufaa ndani ya siku 10 na rufaa ndani ya siku 45 kuanzia tarehe ya uamuzi huu. Imeamriwa hivyo. Imetolewa Dodoma leo tarehe 30 Mwezi Septemba, 2024. F. R. KHALFAN JAJI 30/9/2024 4

Source & reproduction note

Judgment wording, source notices and original paragraph numbers are retained. Esheria supplies the layout and this PDF's page numbers; these are not the source pagination. This is a research copy, not an official or certified court document. Check quotations, citations and publication restrictions against the original source before relying on it.

ORIGINAL SOURCE https://media.tanzlil.org/media/judgment/322501/source_file/6e5012ae8f565f9d/MGAMBWA_SADALA_MCHIWA.pdf

CASE PAGE <https://chat.esheria.ai/case-law/tanzania/Extensionoftime-tanzlil-2024--6a3ea5243b1caa9129819d32>

Prepared on 13 October 2026 · Esheria